# JARIDA LA WAKILI MKUU

ISSN 2686 - 2686 | Toleo la Kumi na Nne | Mei - Julai, 2025




# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAENDESHA MAFUNZO KWA MAWAKILI WA SERIKALI



# BODI YA UHARIRI


## Mwenyekiti

**Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Salmin Hezron Kigondo**

## Wajumbe

**Saddy Rashid Sevingi**
Mkurugenzi Msaidizi Usuluhishi wa Nje

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**CPA Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi Mwandamizi

# Yaliyomo


UK. 04 | Tahariri

UK. 05 | Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri

UK. 06 | Serikali Yashinda Mashauri ya Madai na Usuluhishi

UK. 07 | Taarifa kwa Umma Kuhusu Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali

UK. 11 | Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali

UK. 16 | Wakili Mkuu wa Serikali Ashuhudia Utiaji Saini wa Ushirikiano Kati ya PBA na TLS

UK. 20 | OWMS Yazindua Maktaba Mtandao (E-Library), Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mashauri (CMIS) na Chapa ya Ofisi (Branding Manual)

UK. 26 | Wakili Mkuu wa Serikali Aendesha Kikao cha Faragha kwa Menejimenti ya OWMS

UK. 30 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

UK. 34 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Sherehe za Mei Mosi

UK. 36 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma

UK. 38 | Waziri Mkuu Awaasa Watumishi Kutekeleza Majukumu Yao Kwa Kufuata Sheria na Taratibu za Utumishi wa Umma

UK. 40 | Mfanyakazi Hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Apongezwa

UK. 42 | Wakili Mkuu wa Serikali Afungua Baraza la Wafanyakazi wa OWMS

UK. 46 | Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Washiriki Zoezi la Kupima Afya

UK. 50 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapata Hati Safi

# TAHARIRI



**Prisca Jackson Ulomi**
Mhariri Mkuu

Ndugu msomaji wa Jarida la Wakili Mkuu karibu uungane nasi katika Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu Toleo la 14 kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo yametekelezwa katika kipindi cha mwezi Mei, 2025 hadi Julai, 2025.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na wadau imefanikiwa kutekeleza majukumu ambayo yamekasimiwa kisheria kupitia Tangazo la Serikali Na. 50 la mwaka 2018 lililoanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Ofisi imepewa dhamana ya kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwa ufanisi ili kulinda maslahi mapana ya taifa.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wake ambao ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara mbali mbali, Idara, taasisi, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Mahakama ya Tanzania katika kutekeleza majukumu yake.

Pia, Ofisi hii inashirikiana kwa karibu zaidi na Wizara ya Katiba na Sheria ambayo inasimamia Sekta ya Sheria nchini ili kuhakikisha kuwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii na wadau wengine wa Sekta ya Sheria nchini wanazingatia na kuwezesha utawala wa sheria na kuchangia utoaji na upatikanaji wa haki kwa wananchi.

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2024 hadi mwezi Julai, 2025; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na kutekeleza majukumu yake ya msingi, imeshiriki katika matukio mbalimbali ndanni na nje ya nchi.

Hivyo, nipende kuchukua nafasi hii kuwakaribisha tena wadau wetu na wananchi kwa ujumla kusoma Jarida la Wakili Mkuu Toleo la 14 ili kupata taarifa mbali mbali za utekelezaji na kutoa maoni kuhusu Jarida hili. Niwatakie usomaji mwema. Karibuni!

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Alice E. Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

Ndugu wasomaji na wadau wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Kwa niaba ya Bodi ya Wahariri na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni furaha yangu kubwa kuwakaribisha wote katika jukwaa hili maalumu la habari na taarifa za matukio muhimu ya Ofisi kwa kipindi cha miezi mitatu, mwezi Mei, 2025 hadi Julai, 2025.

Katika jarida hili tumeendelea kuwapa taarifa za utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupitia matukio mbalimbali. Aidha, nipende kuwajulisha kuwa Ofisi imeendelea kupiga hatua na kuboresha miundombinu mbalimbali hususani mifumo ya TEHAMA ili kwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya kuboresha na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki.

Vilevile, Ofisi imeendelea kutekeleza mpango wake wa kuwajengea uwezo Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika maeneo mbalimbali yakiwemo mabadiliko ya sheria, maeneo ya kimkakati mathalani kodi, mafuta na gesi, usuluhishi na uwekezaji, lengo ikiwa ni kuendelea kukuza watumishi kifikra ili kuboresha utendaji kazi.

Ndugu wasomaji na wadau, Ofisi inawahakikishia kuwa itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na uadilifu ili kuendelea kuchangia katika ukuaji wa sekta ya sheria nchini na kulinda maslahi ya Taifa letu.

Ofisi kupitia jukwaa hili, itaendelea kuboresha maudhui yetu na kuhakikisha inatoa taarifa bora na sahihi zenye kuleta matokeo chanya kwa jamii yetu.

Asanteni sana kwa kuendelea kuwa sehemu ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu. Niwatakie usomaji mwema wa Jarida la Wakili Mkuu Toleo la 14.

Kazi iendelee!



# SERIKALI YASHINDA MASHAURI YA MADAI NA USULUHISHI

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2024 hadi Mei, 2025; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshinda mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake  na kuokoa fedha ambazo Serikali ingelipa endapo ingeshindwa mashauri hayo.

Hayo yameelezwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofunguliwa rasmi na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb.) tarehe 03 Juni, 2025. Katika mafunzo hayo, Mawakili zaidi ya 600 kutoka kwenye Wizara, Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walishiriki mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Arusha kuanzia tarehe 02 hadi 04 Juni, 2025.

Dkt. Possi alieleza kuwa mafunzo hayo yamekuwa chachu kubwa katika kuchangia mafanikio ya Ofisi. Alifafanua kuwa baadhi ya mafanikio yanayoonekana wazi ni pamoja na Serikali kuweza kuokoa kiasi kikubwa cha fedha kupitia mashauri mbalimbali yaliyomalizika kwa ushindi upande wa Serikali. Dkt. Possi alitoa mifano ya baadhi ya mashauri hayo na kueleza kuwa kupitia maamuzi ya shauri moja la madai yaliyotolewa na Mahakama Kuu mwezi Mei, 2025, Serikali ilipinga amri ya Mahakama Kuuambayo imeiwezesha kulipwa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 151.5 pamoja na TZS Bilioni 8.5. Aidha, kutokana na maamuzi hayo, Serikali imeepushwa na madai ya zaidi ya TZS Trilioni 2.9.

Sanjari na shauri hilo, alitaja baadhi ya mashauri ambayo yamemalizika kwa ushindi wa Serikali na kuweza kuokoa kiasi kikubwa cha fedha. Mashauri hayo yanajumuisha Shauri la ***M.A Kharafi & Sons Limited dhidi ya Wizara ya Afya na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Shauri la Tanzania Ports Authority na Mwanasheria Mkuu dhidi ya JV Tangerm Construction Co. Ltd na mwenzake.***

Pia, Dkt. Possi ameongeza kuwa Ofisi imeendesha mashauri 70 yaliyotokana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwezi Novemba, 2024 na kushinda mashauri 69 ambayo ni sawa na asilimia 98.6.

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAFUNZO KWA MAWAKILI WA SERIKALI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuendesha Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kila mwaka kwa kuwafundisha mada mbalimbali ambazo zinawajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao kuendana na ukuaji na mabadiliko ya Sekta ya Sheria nchini yanayoendana na matakwa ya kipindi husika katika nyanja ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha mafunzo kwa Mawakili wote wa Serikali kutoka kwenye Wizara, taasisi za Serikali, mashirika ya umma, Ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waliopo nchi nzima kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Mafunzo hayo yalifanyika kuanzia tarehe 02 Juni, 2025 hadi tarehe 04 Juni, 2025 katika ukumbi wa mikutano wa AICC, jijini Arusha.

Taarifa kwa Umma kuhusu kufanyika kwa mafunzo hayo ilitolewa na Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali kwa waandishi wa habari wakati akizungumza nao kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.

Dkt. Possi aliwaeleza kuwa Kauli mbiu ya




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika mwezi Juni, 2025 wakati wa mkutano na waandishi wa habari (hawapo pichani) uliofanyika Jijini Dar es Salaam.*

mafunzo hayo ni, ***“Ubobezi wa Kisheria kwa Ajili ya Kesho: Teknolojia, Mikakati na Mizania Binafsi kwa Mawakili wa Serikali katika Kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050”***.

Dkt. Possi aliongeza kuwa “Hatuna budi kutoa mafunzo ya kimkakati kwa Mawakili wa Serikali ili waendane na mabadiliko mbalimbali katika Sekta ya Sheria ili wanasheria wa Serikali waweze kuwa na utaalam ambao utaboresha uwezo wao wa kitaaluma kuendana na maendeleo ya sasa duniani.”

Kauli mbiu hii iliakisi mafunzo yaliyotarajiwa kutolewa kwa Mawakili wa Serikali kwa kuwa ilizingatia nafasi na majukumu ya Mawakili wa Serikali na tasnia ya sheria kwa ujumla kama nguzo ya maendeleo ya taifa letu kama ilivyoainishwa kwenye moja ya nguzo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayohusu Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani inayolenga nchi yetu kufikia uchumi wa  kipato cha kati ifikapo mwaka 2050.

Vile vile, Dkt. Possi alisema kuwa kupitia mafunzo hayo, Mawakili wa Serikali watajifunza mbinu za kisasa zitakazowawezesha kufanya kazi kwa tija zaidi kwa kutumia teknolojia; watapata maarifa na uwezo wa ziada wa kutoa huduma za kisheria kwa weledi, uadilifu na kwa kuzingatia mabadiliko ya kisheria na ya kijamii yanayoendelea kujitokeza. Hivyo, Mawakili wa Serikali watakuwa na nafasi nzuri ya kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na kuitetea katika vyombo vya sheria kuendana na karne ya 21 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

Pia, Dkt. Possi alisema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuboresha na kuunda mifumo mbalimbali ya kieletroniki inayotumika kwa shughuli za Ofisi ili kuendana na mpango wa Taifa katika matumizi ya TEHAMA ambapo Ofisi itazindua Mfumo wa Menejimenti ya Taarifa za Mashauri (Case Management Information System - CMIS) ambao unasajili mashauri yanayopokelewa na Ofisi, kuhifadhi taarifa mbalimbali za mashauri, takwimu na aina za mashauri yanayoendeshwa kwa kipindi husika.

Aidha, itazindua tovuti na Maktaba Mtandao (Website & e-Library) na Mwongozo wa Chapa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OSG Branding Manual).

Dkt. Possi alitoa rai na kuwaalika Mawakili wa Serikali kushiriki mafunzo hayo muhimu yatakayofanyika kuanzia tarehe 2 mpaka 4 Juni, 2025 ambayo yatafunguliwa rasmi na Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuendesha Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kila mwaka kwa kuwafundisha mada mbalimbali ambazo zinawajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao kuendana na ukuaji na mabadiliko ya Sekta ya Sheria nchini yanayoendana na matakwa ya kipindi husika katika nyanja ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mwisho, WMS alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuandaa mafunzo haya na kuarifu wadau na wananchi kwa ujumla ili Mawakili wa Serikali wapate nafasi ya kushiriki na kujifunza.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika mwezi Juni, 2025 wakati wa mkutano na waandishi wa habari (hawapo pichani) uliofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusu Mafunzo ya Mawakili wa Serikali wakati wa mkutano na waandishi wa Habari uliofanyika Jijini Dar es Salaam*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusu Mafunzo ya Mawakili wa Serikali wakati wa mkutano na waandishi wa Habari uliofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya waandishi wa Habari wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi na vyombo vya habari akizungumza na vyombo vya habari kuhusu Mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha wakati wa mkutano na waandishi wa Habari uliofanyika Jijini Dar es Salaam.*

# MAFUNZO KWA MAWAKILI WA SERIKALI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa na utaratibu wa kuendesha Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kila mwaka kwa kuwafundisha mada mbalimbali ambazo zinawajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao kuendana na ukuaji na mabadiliko ya Sekta ya Sheria nchini yanayoendana na matakwa ya kipindi husika katika nyanja ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa muda wa siku tatu na yalijikita kwenye kauli mbiu isemayo, "Ubobezi wa Kisheria kwa ajili ya Kesho: Teknolojia, Mikakati na Mizania ya Maisha kwa Mawakili wa Serikali katika Kufanikisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050," ambapo Mawakili wanawajibika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yao kwa kutumia mbinu za kisasa na za kimkakati ikiwemo matumizi ya teknolojia ili kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mawakili hao walipata mafunzo kutoka kwa wataalam wabobezi wa ndani na nje ya nchi kuhusu masuala mtambuka ya sheria yakiwemo mafunzo ya Sheria ya Masoko ya Mitaji Tanzania na nafasi ya Mamlaka na Baraza la Masoko la Mitaji katika kutatua Migogoro; Maadili, Uongozi na uaminifu katika utoaji huduma kwa Umma; Nyenzo Muhimu za Wakili wa Serikali; Jinsi Mawakili Watakavyoweza Kujenga Imani Ndani na Nje ya Mahakama; Mikakati Muhimu ya Usimamizi Bora wa Miradi ya Ujenzi; Uelewa wa Fidia na Madai ya Kuvunjwa kwa Mikataba ili Kuleta Ufanisi wa Madai Yanayowasilishwa Mahakamani; Akili Hisia na Jinsi Inavyoleta Umahiri katika Kutoa Huduma Bora za Kisheria; Mbinu za kimkakati za Majadiliano; Sheria katika Dunia ya Kidijitali: Jinsi Teknolojia Mpya katika Sekta ya Sheria Inavyogusa Kazi za Mawakili wa Serikali; na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Aidha, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) alizindua Mfumo wa Menejimenti ya Taarifa za Mashauri; Tovuti na Maktaba Mtandao pamoja na Mwongozo wa Chapa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo kwa pamoja nyenzo hizo zitawawezesha watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati kwa kutumia TEHAMA ili kuwafikia wadau, wateja na wananchi kwa ujumla ili kulinda maslahi mapana ya Taifa.

Ufunguzi wa mafunzo hayo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndugu Samwel Maneno, Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka, ndugu Sylvester Mwakitalu; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Zanzibar, ndugu Shaaban Abdalla; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mhe. Dkt. Joseph Mhagama (Mb); Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo; Mwandishi Mkuu wa Sheria, ndugu Onorius Njole; Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania; na Wakuu wa Taasisi mbali mbali za Sekta ya Sheria nchini.

Mafunzo ya mwaka huu yalijikita kwenye mada mbalimbali zilizogusa mbinu za kisasa na ujuzi wa mifumo ya kisheria unaoendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Kupitia mafunzo hayo, Mawakili wa Serikali walipata nafasi ya kipekee ya kujifunza kutoka kwa wataalamu wabobezi wa ndani na nje ya nchi katika sekta mbalimbali ikiwemo sheria, teknolojia, uongozi na masuala ya kitaifa na kimataifa.

Mawakili walifundishwa mada mbalimbali zikiwemo:-

1. ***Uelewa wa namna bora ya kuendesha majadiliano ili kufikia suluhu nje ya vyombo vya sheria;***
2. ***Uelewa mpana wa sheria za uwekezaji;***
3. ***Uelewa wa fidia na madai ya uvunjaji wa mikataba;***
4. ***Sheria ya Masoko ya Mitaji Tanzania na nafasi ya Mamlaka na Baraza la Masoko la Mitaji katika utatuzi wa Migogoro; na***
5. ***Usimamizi bora wa mikataba ya miradi ya ujenzi.***



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akimkaribisha Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) kufungua Mafunzo kwa Mawakili hao kwa lengo la kuwajengea uwezo yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari akitoa salamu za Ofisi yake wakati wa Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Joseph Mhagama (Mb) akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Serikali wakiongozwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) wakionesha Chapa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kuizindua wakati wa Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha.*


*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati akifungua Mafunzo kwa Mawakili hao kwa lengo la kuwajengea uwezo yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akitoa salamu za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Naibu Mkuu wa Shule ya Sheria kwa Vitendo (Mafunzo, Utafiti na Ushauri), Prof. Clement Mashamba akichangia mada kuhusu namna ya kushughulikia migogoro katika kusimamia masoko ya mitaji wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Mhe. Balozi Obeni Sefue akitoa mada kuhusu Maadili, Uongozi na Uaminifu katika Utumishi wa Umma wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Mawakili wa Serikali kutoka Wizara, Taasisi na Halmashauri za Wilaya na Mikoa, wakimsikiliza Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.*




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Damas Ndumbaro (Mb) (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufungua Mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Mmoja wa wakufunzi wa mafunzo ya Mawakili wa Serikali akipokea tuzo kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Arusha. Kulia anayeshuhudia ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb).*

# WAKILI MKUU WA SERIKALI ASHUHUDIA UTIAJI SAINI WA USHIRIKIANO KATI YA PBA NA TLS




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Waandishi wa Habari wakati wa Hafla ya utiaji saini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS).*

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alishuhudia utiaji saini wa Hati ya Makubaliano (Memorandum of Understanding - MoU) ya ushirikiano baina ya Chama cha Mawakili wa Serikali (Public Bar Association - PBA) na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (Tanganyika Law Society - TLS) uliofanyika tarehe 13 Juni, 2025 kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, jijini Dar es Salaam.

Utiaji saini huo ulifanyika baina ya TLS na PBA chini ya Mkurugenzi Mtendaji wa TLS, Bi. Mariam Othman na Katibu wa PBA, ndugu Rashid Mohamed kwa niaba ya vyama vyao na kushuhudiwa na viongozi wengine akiwemo Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo; Rais wa TLS, ndugu Boniface Mwabukusi; na Makamu wa Rais wa PBA, Bi. Debora Mcharo waliohudhuria hafla hiyo.

Dkt. Possi alisema kuwa PBA na TLS ni vyama vya kitaaluma, wote ni wanasheria na maafisa wa Mahakama, wanahusika katika utoaji haki na wamekuwa wakifanya kazi kwa pamoja, wameona wawe na MoU ili kutekeleza maazimio na matarajio yao.

“Niwapongeze viongozi wa PBA na TLS kwa kufanikisha hatua hii ya kuwa na *MoU*, vyama hivi viwili, PBA na TLS vitashirikiana katika maeneo tofauti ikiwemo kubadilishana uzoefu, ujuzi, mafunzo na Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

tutashirikiana nao kulinda maslahi mapana ya Taifa kwa kuwa watu wachache walifikiri tuna kambi tofauti, sisi ni wamoja, tutaendeleza ushirikiano baina yetu," alifafanua Dkt. Possi.

Naye Rais wa TLS, ndugu Mwabukusi alisema kuwa kupitia ushirikiano baina ya TLS na PBA watatekeleza majukumu kwa pamoja na watashirikiana na Serikali kulinda maslahi ya Taifa. "Wote kwa pamoja tutalitazama Taifa kwa kuwa sheria ni eneo kubwa la kivita kwa sasa kupitia uwekezaji, wanasheria tuna nafasi kubwa kujenga imani na ushirikiano zaidi kwa kuwa nia yetu kubwa ni utawala wa sheria, haki za binadamu, kushirikiana na Serikali katika utungaji wa sheria ili Tanzania iendelee kuwa Taifa la amani, umoja na mshikamano", alisisitiza Mwabukusi.

Akizungumza kwa niaba ya PBA, Makamu wa Rais wa PBA, Bi. Debora Mcharo alisema kuwa utiaji saini wa *MoU* baina ya PBA na TLS utawaunganisha na kuwa na umoja na ushirikiano katika Sekta ya Sheria na watashirikiana kuelimisha jamii ili kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, pamoja na kuelimisha jamii kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025. "Tunaishukuru TLS kuungana nasi kulinda nchi yetu kwa kutumia kalamu katika kutetea maslahi mapana ya Taifa", alisisitiza Bi. Mcharo.




*Katibu wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA), ndugu Rashid Mohamed (aliyekaa kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Bi. Mariam Othuman wakitia saini Hati ya Makubaliano (MoU) wakati wa hafla hiyo iliyofanyika Jijini Dar es Salaam. Wanaoshuhudia nyuma ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama katikati) kulia ni Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) ndugu Boniphace Mwabukusi na wa kwanza kushoto ni Makamu wa Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA), Bi. Debora Mcharo.*




*Katibu wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA), ndugu Rashid Mohamed (aliyesimama kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Bi. Mariam Othuman wakionesha Hati ya Makubaliano (MoU) baada ya kutia saini hati hiyo wakati wa hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam. Wanaoshuhudia ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama), kulia ni Rais wa TLS, ndugu Boniphace Mwabukusi na wa kwanza kulia ni Makamu wa Rais wa PBA, Bi. Debora Mcharo.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo (aliyekaa kushoto) akimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati wa hafla ya utiaji saini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) wakati wa mkutano na waandishi hao uliofanyika Jijina Dar es Salaam.*




*Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), ndugu Boniphace Mwabukusi akizungumza na Waandishi wa Habari wakati wa hafla ya utiaji saini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) na TLS kwenye hafla ya utiaji saini iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali na Chama cha Mawakili wa Tanganyika wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA) na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) wakati wa hafla hiyo iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*




# OWMS YAZINDUA MAKTABA MTANDAO, MFUMO WA USIMAMIZI WA MASHAURI NA CHAPA YA OFISI

## MFUMO WA USIMAMIZI WA MASHAURI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetengeneza Mfumo wa CMIS ambao ni mfumo wa kielektroniki unaohusika na kupokea; kusajili na kuchakata taarifa za mashauri ya Serikali yanayosimamiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Serikali na taasisi zake; kufuatilia mwenendo wa mashauri; kutunza taarifa za mashauri; kupata takwimu za mashauri; kutambua aina ya mashauri, kuandaa ripoti za mashauri; kuhuisha taarifa za mashauri baada ya kutoka mahakamani; notisi za siku 90; na mawasiliano mbali mbali.

Mfumo huu unatumiwa na Mawakili wa Serikali wanapotekeleza majukumu yao ndani na nje ya nchi kwa kuwa unapatikana kwa njia ya kielektroniki hivyo kurahisisha na kufanikisha utendaji kazi, uwazi na uwajibikaji. Mfumo huu ni muhimu kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia kuwa Ofisi hii ni Kampuni ya Uwakili ya Serikali ambayo inasimamia na kuendesha mashauri ya usuluhishi na madai kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwa maslahi mapana ya Taifa.

Hivyo, Ofisi hii imezingatia azma ya Serikali ya Awamu ya Sita inayohimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma.




*Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akitoa maelezo mafupi kuhusu Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Mashauri, tovuti, Maktaba Mtandao na Chapa ya Ofisi hiyo kabla ya kuzinduliwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) (hayupo pichani) kwenye mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha*

## UZINDUZI WA MAKTABA MTANDAO YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imetengeneza tovuti yake yenye anwani *www.osg.go.tz* ambayo ni jukwaa la kuwawezesha wadau na wananchi kupata taarifa mbali mbali kuhusu utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Ndani ya tovuti hii imejengwa Maktaba Mtandao (OSG e-Library) ambayo inawawezesha watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na watumiaji wengine kupata taarifa na rejea za kisheria kwa njia ya mtandao ikiwemo vitabu, maamuzi ya Mahakama, sheria mbali mbali na majarida. Maktaba Mtandao inafanikisha na kurahisisha upatikanaji wa maarifa ya kisheria na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwa kutumia TEHAMA.

Mawakili wa Serikali hutumia Maktaba hii mtandao kufanya utafiti wa kisheria, kuandaa mawasilisho ya Mahakamani na kutetea hoja zao ili kulinda maslahi mapana ya Taifa katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali kwa niaba ya Serikali na taasisi zake. Maktaba Mtandao inapatikana na kutumiwa na Mawakili mahali popote walipo ndani na nje ya nchi katika kutekeleza majukumu yao ya kuitetea Serikali mahakamani.




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili hao kwa lengo la kuwajengea uwezo yaliyofanyika Jijini Arusha. Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (pichani chini) akimkaribisha Mhe. Dkt. Ndumbaro kufungua mafunzo hayo.*



# UZINDUZI WA CHAPA YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekamilisha uandaaji wa Chapa ya Ofisi hii (OSG Branding Manual) ambayo itatumika kuitambulisha Ofisi, kujenga na kuendeleza taswira yake, imani, mtazamo na muonekano wake kwa wadau, wateja na wananchi kwa ujumla wakati wa utekelezaji wa majukumu yake mbali mbali ikiwemo kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Chapa hii itawawezesha watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuitambulisha Ofisi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo muonekano wa mavazi, mawasiliano, mawasilisho na majadiliano wanapoiwakilisha Ofisi kwenye kazi mbali mbali, uandaaji wa nyaraka, mawasiliano baina ya Ofisi na wadau na wananchi ambapo inahusisha njia mbali mbali za mawasiliano kama vile tovuti, mitandao ya kijamii ya Ofisi, machapisho mbali mbali ya Ofisi.

Pia, itawapa mwongozo thabiti watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuzingatia taaluma, weledi, uadilifu na ustadi wa hali juu ili kulinda maslahi mapana ya Taifa katika usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.




*Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akimkabidhi mgeni rasmi, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) Chapa ya Ofisi hiyo kwa ajili ya kuizindua rasmi wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha. Viongozi wengine wakishuhudia tukio hilo.*



*Mawakili wa Serikali kutoka Wizara, taasisi za Serikali nna Halmashauri za Wilaya na Mikoa wakimsikiliza Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Mawakili hao yaliyofannyyika Jijini Arusha. Walioketi mbele ni baadhi ya Mawakili wa Serikali Wafawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliyoratibu mafunzo hayo.*






*Mmoja wa wadau waliodhamini mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Arusha akipokea tuzo kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (pichani juu) baada ya mafunzo hayo kufunguliwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) anayeshuhudia tukio hilo. Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akikabidhi tuzo kwa mdau mwingine kwenye hafla hiyo (pichani chini).*



# WAKILI MKUU WA SERIKALI AENDESHA KIKAO CHA FARAGHA KWA MENEJIMENTI YA OWMS



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Kikao cha Faragha kwa viongozi hao kilichofanyika mkoani Morogoro.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akimsikiliza Mhe. Balozi Peter Kallaghe (hayupo pichani) wakati akitoa mada kuhusu Masuala ya Itifaki Kwenye kikao cha Faragha kwa Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kiichofanyika mkoani Morogoro.*




*Mhe. Balozi Mstaafu, Peter Kallaghe akitoa mada kuhusu Itifaki kwenye kikao cha Faragha kwa Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika mkoani Morogoro.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Mtalaamu wa Uongozi, Bi. Zuhura Muro wakati akitoa mada kuhusu Uongozi, Akili Hisia na Kushughulikia Msongo wa Mawazo wakati wa kikao cha Faragha kwa Wajumbe hao kilichofanyika mkoani Morogoro.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usuluhishi wa Ndani wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu David Kakwaya akichangia mada kuhusu Mawasliano ya Kimkakati Serikalini wakati wa kikao hicho kilichofanyika mkoani Morogoro.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Mtalaamu wa Uongozi, Bi. Zuhura Muro wakati akitoa mada kuhusu Uongozi, Akili Hisia na Kushughulikia Msongo wa Mawazo wakati wa kikao cha Faragha kwa Wajumbe hao kilichofanyika mkoani Morogoro.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbas akitoa mada kuhusu Mawasiliano ya Kimkakati Serikalini wakati wa kikao cha Faragha kwa Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika mkoani Morogoro.*




*Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora, ndugu Camilius Ruhinda akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha Faragha kwa viongozi hao kilichofanyika mkoani Morogoro.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akizungumza na wananchi wakati akizindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyofanyika viwanja vya Maturubai, Mbagala Jijini Dar es Salaam.*

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YASHIRIKI KAMPENI YA MSAADA WA KISHERIA YA MAMA SAMIA

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuunga mkono dhamira njema ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusogeza huduma karibu na wananchi ili kuwahudumia wananchi kwa kutoa elimu na msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Pamoja na zoezi la utoaji wa elimu na msaada wa Kisheria kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zao kwa ufanisi mkubwa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki kampeni hii kwa kujenga uelewa kwa wadau mbalimbali waliotembelea banda la Ofisi hiyo kuhusu masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na lengo la kuanzishwa kwake, namna inavyotekeleza majukumu yake na kuendelea kuainisha tofauti ya utekelezaji wa majukumu yake na kuendelea kuainisha tofauti ya utekelezaji wa majukumu iliyopo kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Aidha, wakati wa kampeni hiyo wadau waliendelea kuelimishwa kuhusu jukumu kuu la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali la kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa dhidi ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Wakati wa kampeni hiyo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilisikiliza na kutatua kero mbalimbali zilizowasilishwa zilizowasilishwa na wananchi wakati wa zoezi hilo ambapo miongoni mwa kero zilizowasilishwa ni masuala ya ardhi na mirathi pamoja na taratibu za kufungua mashauri mahakamani pale mwananchi anapoona hatendewi haki.

Akizungumza mara baada ya ufunguzi wa kampeni hiyo Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Ndugu Camilius Ruhinda alisema kuwa lengo la ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushiriki kampeni hiyo ni kuendelea kutoa huduma za kisheria bila malipo kwa watu wa rika zote bila kujali hali zao za kiuchumi kwa kuendelea kutoa ushauri wa kisheria, msaada wa kisheria katika kufahamu uelekeo wa mashauri na kuandaa nyaraka za kisheria kwa usahihi.

Wakati wa kampeni, njia mbalimbali zilitumika katika kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi hatua iliyosaidia kwa kiasi



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) akizungumza na wananchi walioshiriki uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia uliofanyika katika viwanja vya Maturubai, Mbagala Jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akimsikiliza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) wakati akizindua Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyofanyika katika viwanja vya Maturubai, Mbagala Jijini Dar es Salaam.*

kikubwa kutoa ushauri sahihi kwa wadau na wananchi ikiwa ni pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi na wadau waliofika kupitia njia ya majadiliano.

Uwepo wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia ambayo imefanyika nchi nzima imesaidia kuboresha na kuharakisha upatikanaji wa haki kwa watu wa kipato cha chini na kati ambao mara nyingi walikuwa wakikosa fursa ya kupata haki zao kutokana na gharama kubwa za kisheria hususan za kuendesha mashauri Mahakamani.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia imeendelea kujenga na kuongeza uelewa katika jamii kuhusu haki na wajibu katika kutekeleza masuala ya kisheria, hivyo kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kwa kuongeza ushirikiano miongozi mwa wanajamii na hivyo kusaidia kujenga na kuongeza mshikamano na amani nchini.

Utoaji wa elimu ya msaada wa kisheria umesaidia kukuza uelewa na usawa wa kisheria kwa kuhakikisha upatikanaji wa haki hautegemei hali ya ya kifedha au cheo cha mtu, bali kwa kuhakikisha inapatikana kwa watu wa rika zote bila ubaguzi pamoja na kusaidia makundi ya wananchi wote wakiwemo wanawake, watoto, na wazee ambao mara nyingi wamekuwa hawapati haki zao kwa wakati kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya kisheria.

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ilifunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) katika Viwanja vya Maturubai Mbagala Jijini Dar es Salaam.




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akitoa elimu ya Msaada wa Kisheria kwa mwananchi aliyembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyofanyika kwenye viwanja vya Maturubai, Mbagala Jijini Dar es Salaam.*



*Wananchi walioshiriki uzinduzi wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria wakimsikiliza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) (hayupo pichani) wakati wa uzinduzi huo uliofanyika kwenye viwanja vya Maturubai, Mbagala Jijini Dar es Salaam.*




*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakitoa elimu ya msaada wa kisheria wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyofanyika kwenye viwanja vya Maturubai, Mbagala Jijini Dar es Salaam.*




# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YASHIRIKI SHEREHE ZA MEI MOSI




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) wakati wa Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) yaliyofanyika mkoani Singida.*




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakijiandaa kushiriki maandamano ya Maadhimisho ya Mei Mosi yaliyofanyika mkoani Singida.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) wakati wa Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) yaliyofanyika mkoani Singida.*

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YASHIRIKI UFUNGUZI




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Nicodemus Agweyo akitoa elimu ya msaada wa kisheria wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa na bango la kauli mbiu kuhusu Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kushiriki ufunguzi wa Maadhimisho hayo yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja baada ya ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akizungumza na watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali wakati akifunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

# WAZIRI MKUU AWAASA WATUMISHI KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO KWA KUFUATA SHERIA, TARATIBU ZA UTUMISHI WA UMMA

Watumishi wa umma kutoka Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Halmashauri za Wilaya na Mikoa kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kufuata Sheria, Kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Wito huo umetolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) wakati akifunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.

Akizungumza mbele ya viongozi wa serikali, watumishi wa umma na wananchi waliojitokeza kushuhudia maadhimisho hayo, Mhe. Majaliwa alisema kuwa Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa umma, huku akiwasisitiza kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuleta maendeleo kwa kutoa huduma zenye tija na manufaa kwa wananchi.

Mhe. Majaliwa aliongeza kuwa ni vyema kila taasisi ya umma kuweka mikakati ya kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kutumia fursa za uwepo wa maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma ili wajitokeze kwa wingi na kupata huduma zinazotolewa na Serikali kwa wakati.

Mhe. Majaliwa aliendelea kuwaasa watumishi wa umma kote nchini kujisajili katika mfumo wa kidijitali wa e – wezesha, ambao unawezesha watumishi wa umma kuwekeza moja kwa moja kupitia makato ya mshahara au mapato mbalimbali ya biashara kwa ajili ya kuandaa mazingira bora ya kiuchumi pale wanapomaliza muda wao katika utumishi wa umma.

Katika kuunga mkono maadhimisho hayo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, iliungana na taasisi mbalimbali za umma kushiriki katika maonesho hayo yaliyofanyika kwa wiki nzima ambapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitumiaadhimisho hayo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu majukumu yake ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa Mashauri ya Madai, Usuluhishi, Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi ndani na nje ya nchi.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitumia maonyesho hayo kuendelea kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa watumishi wa umma na na wananchi walioshiriki maadhimisho hayo ambapo masuala mbalimbali yaliyopatiwa ufumbuzi ni pamoja na masuala ya kiutumishi, mirathi, taratibu za kufungua shauri na tofauti iliyopo kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma huadhimishwa kila mwaka barani Afrika kuanzia Juni 16 hadi 23, yakihusisha taasisi mbalimbali za umma kuonesha huduma na mafanikio yao kwa wananchi ambapo Maadhimisho ya mwaka huu yanaongozwa na kaulimbiu: “Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijitali ili Kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na Kuchagiza Uwajibikaji”, kaulimbiu inayolenga kuhimiza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kuboresha huduma kwa wananchi na kuimarisha uwajibikaji wa watumishi wa umma.

*Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja baada ya hafla ya kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Boniphace Simbachawene (Mb) akizungumza na watumishi wa umma wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali wakati wa kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




# MFANYAKAZI HODARI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI APONGEZWA

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imempongeza Afisa TEHAMA wa Ofisi hiyo ndugu Mussa Yonah kwa kuchaguliwa na watumishi wa Ofisi na kupittishwa na Menejimenti ya Ofisi hiyo kuwa Mfanyakazi hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2025.

Serikali Bi. Alice E. Mtulo kwa niaba ya watumishi na menejimenti ya Ofisi hivyo wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali uliofanyika Jijini Arusha.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Bi. Mtulo alieleza kuwa ndugu Yonah alichaguliwa na Wajumbe wa Menejimenti baada ya kushindanishwa na watumishi wengine kutoka idara na vitengo tofauti vya Ofisi hiyo katika uchaguzi uliozingatia sifa na vigezo vilivyowekwa.

Amezitaja sifa hizo kuwa ni pamoja na kutunza siri za Ofisi, kufanya kazi kwa weledi na uadilifu, kufika kazini kwa wakati, kuwa

nadhifu, kutekeleza majukumu yake kwa wakati na mapangilio, mahusiano mazuri na watumishi wengine, kujiepusha na vitendo vya rushwa, kuwa mbunifu na tayari kusikiliza maoni na ushauri kutoka kwa wengine bila malalamiko na kuzingatia sheria za utumishi wa umma wakati wote awapo mahala pa kazi.

Bi. Mtulo amewasihi watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na uadilifu huku wakizingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma katika kuwahudumia wananchi kwa ustawi wa taifa.

Akimzungumzia Bw. Mussa Yonah, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ambaye pia ndiye Mkuu wa Mamlaka ya nidhamu na Afisa Masuuli ofisini hapo Bi. Alice E. Mtulo alisema kuwa mtumishi huyo alistahili kuwa Mfanyakazi hodari kwa mwaka 2025 kwa kuwa amekuwa akitekeleza majukumu ya Afisa TEHAMA kwa weledi na umahiri mkubwa katika kuwahudumia wananchi na watumishi wenzake wanaohitaji kupata huduma za TEHAMA ofisini hapo bila upendeleo na ubaguzi wowote na kwa wakati.

Alifafanua kuwa ushindi wa ndugu Yonah ni chachu kwa watumishi wengine walioko kazini hasa watumishi wapya ambao ndio wameanza kazi huku akitoa wito kwa viongozi wa Ofisi hiyo kuendelea kuwaamini vijana kwa kuwa ndio nguvu kazi ya taifa wanaoweza kufanya kazi kwa nguvu, weledi na ufanisi zaidi katika kuhakikisha wanailetea maendeleo ofisi hii na taifa
kwa ujumla.

Naye, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Azizi Makaburi amemuelezea ndugu Yonah kuwa ni mtumishi jasiri, mahiri na mwenye kujitolea na anayefanya kazi kwa bidii katika kila jukumu analopewa na kuitekeleza kwa wakati.

Ameongeza kuwa nidhamu ya kazi aliyonayo mtumishi huyo imechangia kwa kiasi kikubwa kumfikisha kwenye mafanikio hayo na kuibuka kuwa mfanyakazi hodari miongoni mwa watumishi wengine alioshin- danishwa nao huku akimsihi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kwa kuwa bado ni kijana ana safari ndefu na jukumu kubwa ambalo ni kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kutumia ujuzi wake wa masuala ya TEHAMA kwa lengo la kuiletea nchi yetu maendeleo.

Kwa upande wake ndugu Yonah akizungumza baada ya pongezi hizo amewashukuru watumishi na uongozi wa Ofisi hiyo kwa kutoa miongozo kwa watumishi hao ambayo imekuwa dira katika kutoa muelekeo wa Ofisi hiyo katika kusimamia maadili, kufanya kazi kwa bidii na weledi katika kulitumikia taifa. Hivyo, imemfanya kuwa mfanyakazi hodari wa Ofisi hiyo kwa mwaka 2025.

Ndugu Yonah aliendelea kuwashukuru watumishi wenzake kwa kutambua mchango wake na ameahidi kuendelea kujituma na kufanya kazi kwa bidii ili kuendelea kutoa huduma zenye viwango vya hali ya juu kwa watumishi wenzake na wadau wengine wanaopatiwa huduma katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Ndugu Yonah amewaahidi watumishi na Menejimenti ya Ofisi hiyo kuendelea kuwa mwadilifu, mwaminifu na mzalendo katika kipindi chote cha utumishi wake ndani na nje ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuendelea kuwa mfano kwa watumishi wenzake ndani ya Serikali.




# WAKILI MKUU WA SERIKALI AFUNGUA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OWMS




***Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akimkaribisha Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) kufungua Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Jijini Dodoma.***




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akiwaongoza wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuimba wimbo wa mshikamano daima wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Jijini Dodoma.*



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiimba wimbo wa mshikamano daima wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akizungumza na wajumbe wa Baraza la Ofisi hiyo wakati wa mkutano wao uliofanyika Jijini Dodoma.*



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza kwa makini Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati akifungua mkutano wa Baraza la Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Dodoma.*

# WATUMISHI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI WASHIRIKI ZOEZI LA KUPIMA AFYA



*Mratibu wa Usimamizi wa Magonjwa yanayoambukiza wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dkt. Aisha Zukheri akitoa mada kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhusu magonjwa hayo wakati wa mafunzo ya masuala ya afya yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wamehamasishwa kujenga tabia ya kupima afya zao kila wakati hatua itakayowasaidia kupata ushauri sahihi kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa na yanayoambukizwa ikiwemo VVU na UKIMWI.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Madai ya Nje, Bi. Vivian Method, wakati akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice E. Mtulo kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa hayo kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Bi. Method alieleza kuwa kupima afya mara kwa mara kutasaidia watumishi hao kujua hali ya afya zao pamoja na kupata elimu sahihi ya masuala ya afya itakayowasaidia kujikinga na magonjwa hayo hasa VVU sambamba na kubadili mtindo wa maisha kwa watumishi hao.

Amesisitiza kuwa uamuzi wa watumishi wa Ofisi hiyo kupima afya zao kutawasaidia kwa kiasi kikubwa kujiepusha na magonjwa

sugu kama vile VVU, kisukari, Shinikizo la Damu, Kiharusi, Ugonjwa wa Figo, Ini na magongwa mengine mengi yanayoambukizwa kwa njia ya kujamiana.

Kiongozi huyo aliendelea kuwashauri watumishi hao kuendelea kufuatilia taarifa sahihi za namna ya kujikinga na Magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza kama vile VVU/UKIMWI, ili kupata taarifa sahihi ili waweze kusaidia kutoa elimu ya kujikinga na maradhi hayo kwa wananchi na jamii kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa zoezi la upimaji afya kwa watumishi hao Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Bi Asha Hayeshi amesema kuwa zoezi la kupima afya ni muhimu kwa watumishi waliopo kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwa watumishi hao hukosa muda wa kuchunguza afya zao katika vituo vya afya kutokana na kuwa na majukumu mengi ambayo yamekuwa yakichukua muda wao mwingi.

Bi. Hayeshi alieleza kuwa wameamua kuendesha zoezi la upimaji wa afya kwa watumishi kwa kuzingatia ukweli kuwa kama mtumishi atakuwa na afya njema ataweza kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na hivyo kuisaidia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kufikia malengo iliyojiwekea kuendana na mpango kazi.

Kwa upande wake Mratibu wa zoezi la kupima afya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu Geofrey Annania alisema kuwa watumishi wanatakiwa kupima afya zao ili waweze kufahamu namna wanavyoweza kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa kwani limekuwa janga kwa jamii kwa sababu ya kukosa muda wa kufanya mazoezi, kuangalia afya zao na mtindo wa maisha usiofaa.

Wakizungumza mara baada ya kupima afya zao baadhi ya watumishi walioshiriki zoezi hilo waliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuendesha zoezi hilo kwa kuwa limewawezesha kupata nafasi ya kujua hali ya afya zao na sasa wataweza kuishi kwa kuchukua tahadhari kulingana na maelekezo na ushauri walipata kutoka kwa wataalamu hao.

Mbali na kuendesha zoezi la kupima afya za watumishi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitoa elimu kuhusu masuala ya lishe na afya iliyotolewa na Kaimu Afisa Lishe wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, Bi. Neema Mwakasege, elimu kuhusu masuala ya VVU na Ukimwi iliyotolewa na Dkt. Aisha Zukheri kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Jiji la Dar es Salaam, elimu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza iliyotolewa na Mratibu wa Kusimamia Magonjwa yasiyoambukiza wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, Dkt. Milka Mathania.

Kupitia huduma hiyo watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walishiriki zoezi la kupima huduma ya afya kwa kupima uzito wa mwili (BMI), kupima kiwango cha sukari (RBG) na kupima maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mafunzo hayo ni muendelezo wa mpango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoa elimu na kuwahamasisha watumishi wake kupima afya zao mara kwa mara ikiwa ni hatua ya kuwaongezea watumishi hao uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kiafya ikiwa ni pamoja na kuwajengea hali ya kujiamini wawapo mahala pa kazi.

Vilevile, mafunzo hayo yalitolewa ili kufanikisha utekelezaji wa malengo mtambuka ya Serikali ambayo ni kupunguza maambukizi ya VVU, UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza na kuboresha huduma za lishe.



*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Mratibu wa Kusimamia Magonjwa Yanayoambukiza wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dkt. Aisha Zukheri (hayupo pichani) wakati akitoa mada kuhusu magonjwa hayo wakati wa mafunzo kwa watumishi hao yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*




*Mfano wa kifaa tiba kinachojulikana kitaalam kama Kipimajoto cha Shinikizo la Damu (Blood Pressure Monitor) ambacho kilitumika kufanya vipimo kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa mafunzo kuhusu afya yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*





*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakichangia mada kuhusu Lishe na Afya wakati wa mafunzo kuhusu afya yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*





*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakipimwa shinikizo la damu wakati wa mafunzo kuhusu afya yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*





*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakipima uzito wakati wa mafunzo kuhusu afya yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



**Bi. Alice E. Mtulo**
*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali*



**Dkt. Ally Possi**
*Wakili Mkuu wa Serikali*



**CPA Devota Ngulugulu**
*Mhasibu Mkuu - OWMS*

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAPATA HATI SAFI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepata Hati safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kipindi cha miaka sita (6) mfululizo tangu kuanzishwa kwa Ofisi hii mwaka 2018 hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2024/25. Mwaka wa Fedha 2024/25; Ofisi ilitengewa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 24.5 (24,574,962,600) ambazo zilitumika kwa ajili ya mishahara, uendeshaji wa Ofisi, uratibu, usimamzi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi na mafunzo mbali mbali kwa Mawakili wa Serikali ikiwemo masuala ya uchaguzi.

Ofisi imefanya matumizi ya fedha tajwa hapo juu kuendana na mgao wa fedha wa kila mwezi unaowasilishwa kutoka HAZINA na kuiewezesha Ofisi kutekeleza majukumu ya msingi ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ya ndani na nje ya nchi pamoja na majukumu mengine ya uendeshaji wa ofisi, mafunzo ya kuwajengea uwezo na utaalam watumishi, ununuzi wa vitendea kazi mathalani magari, kompyuta, kuweka mazingira bora na wezeshi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na miundombinu ya mifumo ya TEHAMA.

Upatikanaji wa hati safi umetokana na dhana ya uwajibikaji wa pamoja na uwazi uliopo baina ya Menejimenti na watumishi wa Ofisi ambapo fedha zinatengwa na kuridhiwa matumizi yake baada ya kufanyika kwa kikao cha Kamati ya Bajeti.

Kikao hicho hufanyika kila mwezi ambapo wajumbe ni Wakuu wa Idara na Vitengo wenye kasma na vifungu vyenye majukumu na tengeo la fedha kadri ilivyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendana na mpango kazi wa Ofisi.

Ofisi imejiwekea utaratibu wa kufanya kikao kila wiki kwa Wakuu wa Idara na Vitengo

kwa lengo la kujadili, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi na uendeshaji wa Ofisi ili kupata mrejesho wa hatua iliyofikiwa katika kuhakikisha kuwa majukumu husika yanatekelezwa kwa wakati ili kuongeza tija na ufanisi.

Vile vile, Ofisi inazingatia maelekezo ya Sheria, Kanuni, taratibu na miongozi ya fedha inayotolewa kila mwaka yenye maelekezo ya matumizi ya fedha kwa Idara na taasisi za Serikali ili kuhakikisha matumizi hayo yanaakisi mahitaji ya wananchi na malengo ya Serikali kwa ujumla.


Pia, Ofisi inazingatia miundo mbalimbali ya Serikali kwa ajili ya kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali. Miundo hiyo ni pamoja na Kamati ya Ukaguzi, Kitengo cha Ugavi na Manunuzi, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.

Miundo hiyo hutumia mifumo mbali mbali kama vile mfumo wa NEST, GAMIS katika utunzaji na uchakataji wa uchakavu wa mali za Serikali na Mfumo wa Uhasibu Serikalini (Muse) ambayo yote kwa pamoja inatumia TEHAMA.

Uwepo wa mifumo hiyo inabeba jukumu la kuwa jicho la Afisa Masuuli ili kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha yanaendana na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa; yanazingatia sheria ya fedha na ya manunuzi.

Aidha, kumekuwepo na ushirikishwaji wa wafanyakazi kupitia vikao vya Baraza la Wafanyakazi, vikao vya watumishi wa Idara na vitengo na Mkutano Mkuu wa mwaka wa watumishi wote. Wajumbe wa Baraza hilo na mkutano huo wanapata fursa ya kupitia mipango, majukumu na utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Ofisi inafikia malengo iliyojiwekea ya kuiwakilisha Serikali na taasisi zake kwenye mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Hivyo, ni matumaini ya Kitengo cha Uhasibu na Fedha kuwa dira na azma iliyowekwa itaendelea kutimizwa ili Ofisi iendelee kupata hati safi.

Nitoe kongole kwa Mkuu wa taasisi, Afisa Masuuli, menejimenti na watumishi wote kwa kupata hati safi kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Kazi Iendelee!


REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL AUDIT OFFICE

OFFICE OF SOLICITOR GENERAL

REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ON THE FINANCIAL AND COMPLIANCE AUDIT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2024

Controller and Auditor General,
National Audit Office,
"Ukaguzi" House,
4 Mahakama Road,
P.O. Box 950,
41104 Tambukareli,
Dodoma, Tanzania.
Tel: 255 (026) 2161200-9,
E-mail: ocag@nao.go.tz
Website: www.nao.go.tz

March 2025

AR/CG/19/OSG/2023/24


1.2.2 Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines

Subject matter: Budget formulation and execution

I performed a compliance audit on budget formulation and execution in the Office of Solicitor General for the financial year 2023/24 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.

Conclusion

Based on the audit work performed, I state that Budget formulation and execution of the Office of Solicitor General is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic ofTanzania
March 2025

Controller and Auditor General | AR/CG/19/OSG/2023/24 | 4

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |